Kongamano la Kiswahili Bayreuth

UNIVERSITÄT BAYREUTH

Mwaliko wa

# KONGAMANO LA KISWAHILI LA THELATHINI NA MOJA

Bayreuth tarehe 11 hadi 13 Mei 2018

Wenzetu wapendwa, wapendwa washiriki, ndugu na marafiki,

Ni furaha yetu kuwaalikeni nyote kwa Kongamano la Kiswahili la thelathini na moja litakalofanyika Bayreuth kuanzia tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi wa tano mwaka wa 2018. Kongamano letu ni mkutano wa kipekee wa kila mwaka utoao fursa kwa yeyote yule aliye mtaalamu wa masomo mbalimbali yanayohusu utafiti na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vya lugha ya Kiswahili, fasihi na tamaduni za Afrika Mashariki. Msingi huu wa kongamano letu mjini Bayreuth, unaojikita katika nyanja na mada maridhawa, huwa ni fursa kwa wengi kujuzana kuhusu tafiti zinazoendelea. Hivyo basi, tunawakaribisheni tena wote ambao huja hapa Bayreuth mwaka baada yamwaka na pia tutafurahi sana kuwapokea na kuwakaribisha wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya katika kongamano lijalo.

**Mada kuu ya kongamano la 2018**

Kama ilivyo kawaida, pia kongamano la thelathini na moja lina mada kuu. Mada yake ni **mtandao**. Lakini hatutaki kuchukua mtandao kama tafsiri ya neno la Kiingereza “internet” peke yake, ila kama njia ya kuangalilia jamii, haswa mahusiano ya watu, matumizi yao ya lugha na namna ya kuwasiliana na kuandika fasihi. Kwa hiyo, zaidi ya maana finyu ya *internet*, tunapendekeza kutumia dhana pana ya mtandao kwenye mijadala yetu. Dhana hizi ni zilizopata umuhimu katika taaluma na fani nyingi, haswa elimu jamii *(social sciences na cultural studies)* tangu miaka tisini. Mtandao ni dhana inayosisitiza mahusiano na mawasiliano kwa njia maalum: tofauti na dhana nyingine, kama kwa mfano dhana ya mti *(tree-model)* ambayo inashikilia kuwa chimbuko ni moja lakini matawi ni mengi. Kwenye mtandao kila fundo (mfano wa fundo la wavu) linahusiana na mafundo mengine hadhi ikiwa sawa. Hakuna umuhimu zaidi wa fundo lolote kama fundo-kitovu, lakini kuna mahusiano tu.

Kwa hivyo, tunapendekeza dhana hii ya mtandao ili tujadiliane mahusiano ya wasemaji wa Kiswahili wanaoishi nje ya Afrika Mashariki na wale ambao wapo Afrika Mashariki: wanajenga mahusiano ya aina gani? Mtandao unatualika kuangalia mifumo ya mawasiliano baina ya watu wanaozungumza lugha zaidi ya moja na pia inatufanya tusisitize zaidi matumizi ya lugha (na tusiuchukue kama mfumo usiobadilika). Pia, inatutia moyo kuangalia fasihi kutoka kipengele hicho: Je, mtandao unatupatia njia ya kuziangalia upya majaribio ya waandishi ya kuandika? Ama inatuletea mtazamo mpya kuhusu fasihi simulizi inayobadilika kila wakati kulingana na uhusiano na mazingira yake? Wasemaji wa Kiswahili na waandishi wa Kiswahili wanatumia mbinu gani au wanaibua mitindo ipi katika mawasiliano yao?

Hatimaye, mwangalio huu vilevile unatubidi tuangazie na uhusiano baina ya watu kwa upande mmoja na teknologia kwa upande mwingine: Wasilisho zenye michango kuhusu umuhimu wa mtandao kwa maana ya internet na tovuti za jamii inakaribishwa. Je, watu wanajengaje mahusiano kimataifa – yaani mahusiano ya kuvuka mipaka ya nchi na hata bara? Mifumo ya mawasiliano inabadilika vipi? Je, mtandao unaleta njia gani mpya za kuwasiliana? Je, mtandao unasaidia kwa kutoa fursa za kubadilishiana mawazo ambayo hayapati nafasi katika mbinu za habari zilizopo, ama inazidi tu kuongeza au kukuza mipaka baina wanaoweza kutumia mbinu hizi na wasioweza kwa kukosa uwezo, uwe kifedha au kielimu, ili kuzitumia? Vilevile, tunakaribisha wasilisho zilizo na mielekeo ya kihistoria: mtandao kwa maana ya uhusiano wa watu, teknolojia, lugha na matini si jambo la usasa ama utandawazi: kwa karne nyingi, kwa mfano, miswada na majahazi viliunganisha watu kutoka pande zote za Bahari ya Hindi na baadaye, uchapishaji pia ulikuwa ni mbinu muhimu ambayo iliwezesha njia mpya za mawasiliano.

**Mada nyingine**

Tunapendekeza mada kuu ya hapa juu, iwe ndiyo mada kati ya kujengea mijadala yetu kwenye kongamano la 2018, lakini kama wengi wetu tujuavyo, Kongamano la Kiswahili Bayreuth halitaki kubana washiriki katika sehemu zilizotajwa tu. Kwa hiyo, pia tunawaulizeni msisite kupendekeza michango mingine ya vipengee vinavyorejelea lugha, fasihi au tamaduni za maeneo ya Kiswahili; kwani Kongamano la Bayreuth linalenga nyanja tofauti tofauti na vile vile ni fursa iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayohusu Kiswahili, Uswahili na Waswahili kwa jumla.

**Usajili**

Tafadhali tumeni makala katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kila wasilisho litapewa muda wa dakika thelathini tu; ambamo dakika ishirini ni za kuwasilisha na dakika kumi ni za majadiliano na hadhira. Tafadhali jiandikishe kwa baruapepe kupitia *swahili@uni-bayreuth.de* na ututumie kichwa (angaa cha awali) cha makala au mapendekezo ya paneli mpaka **tarehe 30 Desemba mwaka 2017**. Iwapo utawasilisha kwa Kiswahili, tutumie pia muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala, ili tuweze kupanga vizuri.

**Pahala na Wakati**

Pahala pa Kongamano hili ni Iwalewahaus, kituo cha masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth, iliyoko kwenye Wölfelstraße 2, kuanzia tarehe 11 Mai hadi 13 Mai 2018.

Wasilianeni nasi bila kusita iwapo mna maswali yoyote. Kwa mambo yote yanayohusu kongamano tafadhali tumieni anwani yake ya barua pepe, yaani *swahili@uni-bayreuth.de*

Karibuni nyote!
Salamu nyingi,
Ni watayarishi wenu
Nikitta Adjirakor, Fred Bosire, Duncan Tarrent, Annachiara Raia na Clarissa Vierke

Swahili Colloquium
Prof. Dr. Clarissa Vierke

Literaturen in afrikanischen Sprachen
Universität Bayreuth
95440 Bayreuth
Telefon: + 49 921 55-3550
Fax: + 49 921 55-3641
Email: swahili@uni-bayreuth.de
http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/